

# HATARI, HAKI ZA USALAMA KATI- KA BAHARI 03

Bahari ya Aegean

Brosha ya maelezo hii ni kwa watu wanaofikiria kuvuka bahari ya Aegean kati ya Ugiriki na Uturuki. Kuvuka kihramu ni uhalifu katika Ugiriki na Uturuki na ni kwa vyo vyote vile hatari. Andiko hili halina lengo kutisha au kuhimiza watu kujaribu kuvuka lakini kutoa maelezo bila kupendelea upande wo wote kuhusu hatari, haki na hatua za usalama muhimu kuzingatia ukiwa baharini. Tunatumaini kwamba maelezo ya andiko hili inaweza kuokoa maisha yako lakini ujue haitafanya kivuko salama zaidi.

Tangu miaka ishirini, Jumuiya ya Ulaya ilikataa maombi ya viza mengi sana. Sawia vita, migogoro na umaskini zinalazimisha watu wengi kukimbia kutoa nchi zao na wanatumaini kutafuta usalama katika Ulaya. Ijapo upungufu wa nafasi halali kufika eneo la Ulaya na ijapo hatari inayohatarisha maisha watu wengi wa nyinyi wanaamua kukimbia na kuvuka mpaka wa bahari.\*

---

\* Alngawa brosha ya maelezo hili inazingatia hasa hali mpakani wa bahari, baadhi ya maelekezo yenye manufaa kwa watu pia wanaozingatia kuvuka mpaka wa bara katika eneo la Evros.

Simu ya kin'gora



+ 334 86 51 71 61

## KABLA YA KUONDOKA NA BOTI, SOMA MAELEKEZO HAYA: Kwa kweli unataka kuhatarisha maisha yako?

Una hakika kwamba unataka kuhatarisha maisha yako utakapovuka mpaka wa bara au bahari? Kila mwaka, kufuata mpaka wa Ugiriki-Uturuiki kati ya 150 na 200 vifo vinathibitishwa kwa wastani lakini inaelekea kwamba idadi ya kweli ni kubwa zaidi. Miaka ya mwisho kulikuwa na ripoti nyingi za watu waliokamatwa na askari wa pwani wa Ugiriki na waliofukwa kiharamu kurudi Uturuiki. Hii ni hali hatari pia.

### Uhalifu wa uhamiaji haramu

Kiingilio halali cha Ugiriki kwa watu ambao hawana passporti ya Jumuiya ya Ulaya kinahitaji viza. Bila viza mara nyingi wahamiaji wanatendwa kama wahalifu. Kama wanakukamata ukiondoka Uturuiki kiharamu na bila ruhusa, utashtakawa kwa uhalifu wa kuingilia au kuondoka kihalifu Uturuiki. Faini ni kati ya 1000 na 2000 TL kama aya 102/a ya Sheria ya Wageni na Ulinzi wa kimataifa inasema (Sheria Nambari 6458 ya 04/04/2103). Tafuta maandishi ya sheria (kiingereza) hapa: <http://tinyurl.com/lr22p7m>

## UKIAMUA KUONDOKA, SOMA HICHO:

Kwa kawaida kivuko kinatokea usiku, botini ambao ni mdogo na inayopakawa na watu mno. Baadhi ya boti zinazama au zinapinduka kwa ajili ya hali ya hewa mbaya, kiwewe botini, au kwa sababu boti ni mzee na zina hali mbaya. Imesharipotiwa pia kwamba watumishi wa mpaka walisukuma wakimbizi kurudi ambapo walipokuja au walitumia nguvu na wakati huo huo wanasababisha hatari kwa wakimbizi. Mara nyingi boti baharini haziji kuokoa wakimbizi hatarini hata kama wanawaona. Maelekezo yanayofuata hayafanyi kivuko salama zaidi. **Inawezekana pia kwamba wewe ni katika hali fulani na huwezi kufuata madokezo haya, kwa mfano kapteni wa boti yako hakuruhusu kufanya hivyo. Kwa vyo vyote vile, brosha hii inakupa mawazo kuhusu utazamie nini na ujiandae vipi. Mkijipanga kama vikundi na mnajiandaa kwa kivuko, athari yenu kuamua ni kubwa zaidi. Maelekezo haya yanguweza kuokoa maisha yenu.**

## **Nunua kizibao cha ukombozi na ulishaji**

- Angalia kwamba kuna vuzibao uya ukombozi uinauyotosha kwa watu wote botini. Kabla ya kuingia boti unaweza kununua kizibao kwa 30 Turkish Lira. Kivae ukiingia boti na kivae wakati wote botini;
- Hatari ya kuanguka baharini au kuloa kabisa ni kubwa sana. Fungasha vitu uya thamani uyako uyote mfukoni wa plastiki na wavae mwilini. Zingatia kwamba vitu uyote huuyovai mwilini vina nafasi kupotezwa. Kwa kuwa vitu uyako vina nafasi kupotezwa au kuibiwa, piga fotokopi ya vitu muhimu kama hati unazohitaji kama thibitisho kwa ombi la kimbilio lako;
- Chukua maji na chakula botini;
- Vae nguo zinazofaa kwa msimu, lakini usisahau kuchukua nguo kwa kupata moto na koti yenye kutopitisha maji.

## **Angalia kwamba vifaa uya dharura vinafanya kazi**

- Angalia kwamba kuna ishara za dharura na maonyo botini! Roketi za ishara (?) na madeba ya moshi zinaweza kuokoa maisha yenu. Kwa uyo uyote vile vitu uyote vinauyoweza kusababisha makini uangalifu wa watu uyenye manufaa: filimbi, nguo zenye kung'aa, mifuko ya plastiki, vioo, simu au flashi ya kamera, tochi na kadhalika.

## **Cheki simu yako**

- Maeneo mengi ya bahari ya Aegean yana mtandao wa simu. Simu zinaweza kuwa vifaa muhimu kuita msaada au kuripoti majambo ya kurudishwa na watumishi wa mpaka.
- Angalia kwamba simu yako imechajiwa na ina vocha inayotosha kupiga baadhi ya simu ya kimataifa (angalau 50 TRY). Kwa kawaida unasemwa kutotumia simu yako ukiuuka mpaka, kwa hivyo simu zimezimishwa kwa kawaida. Ifungie mfukoni wa plastiki wenye kutopitisha maji kuilinda dhidi ya maji ya bahari. Hatua hizi zinataabisha kutumia simu yako. Bali, ikiwezakana simu yako ishikwe mwilini wakati wote na mahali penye kifika kirahisi ili jambo likitokea unaweza kuichukua kupiga simu kwa msaada na kuitumia kuripoti inatokea nini.
- Nambari broshani hii.
- Chukua nambari za simu za ndugu na marafiki zako wanaoishi Uturiki na/

au Ulaya, na waambie kuhusu safari yako kabla ya kuondoka ili waweze kipigia huduma ya dharura wasiposikia na wewe. Ukiwana na smartphone unaweza kudaunilodi apps zinazokuwezesha kugawanya majira ya nukta yako (kwa mfano: **One Touch SOS**: <http://tinyurl.com/lwc8pjl>, kwa Android; na **SOS My Location** <http://tinyurl.com/l3ovg29> kwa Iphone). Pia unaweza kutuma mahali pako ukitumia Whats App na Viber. Unaweza kutuma majira ya nukta yenu nambari hii (+ 49 163 5024825) mkiwa na dharura, kama wewe ni mhanga wa kurudishwa (kurudushwa kiharamu na watumishi wa mpaka). Kupiga namba ya simu hii hairuhuswi. Ukitaka kupiga simu piga namba ya kin'gota: 0033 486 517 161 (Angalia sanduku).

- Mkimeshaonwa na mtumishi wa mpaka wa Ugiriki unaweza kutumia simu yako hali ikifaa. Ukifikri unaiweza kutumia wakati watumishi wapo pigia simu watu wengi sana kuwaeleza hali na mahali kwetu.

## **Angalia utabiri wa hali ya hewa ya mahali pa kuondoka na kufika**

Angalia katika intaneti kwamba hali ya hewa ni nzuri sana kwa siku mbili zitakazofuata kwa mahali pa kuondoka na kufika. Vyanzo vyenye kujulikana ni:

- <http://meteo.gr/meteoplus/sailingmaps.cfm>
- [http://poseidon.hcmr.gr/waves\\_forecast.php?area\\_id=aeg](http://poseidon.hcmr.gr/waves_forecast.php?area_id=aeg)

## **Usiingie botini inayojazwa na watu wengi mno au inayoharibika**

- Angalia kwamba kiunzi cha boti kina hali nzuri: isiwe na mashimo na sehemu zenye kuharibika! Boti ikiwa na hali mbaya maisha yenu yanahatarishwa.
- Kwa wastani, boti yenye urefu wa mita kumi haiwezi kuchukua zaidi ya watu kumi. Namba hii inaenda mpaka watu 30 kwa boti yenye urefu wa mita 20. Boti inayojazwa na watu mno ina uwezekano mkubwa kuzama.
- Angalia kwamba kuna petroli inayotosha urefu wa mara mbili ya safari!
- Angalia kwamba kuna makasia yanayotosha na kwamba yana hali nzuri.

# BAHARINI

---

## Hatua za kukinga wakati wa safari

- Angalia kwa makini na jaribu kuripoti (kwa mfano kwa kuandika) zote inazotokea au unazooona wakati wa safari. Taarifa zote kuhusu mahali na wakati zenye manufaa kwa dharura. Andika mihtasari, piga picha na chukua GPS majira ya nukta ikiwezekana. Angalia mazingira kwa mawe makubwa na boti nyingine zinazoweza kusababisha migogano!
- Jikinga dhidi ya ubaridi. Jaribu kutoloa!
- Usizurure botini kwa usawa wa boti!
- Wakati wa safari utulie na epuka migogoro! Msaidiane na mkingana maisha ya watu wote. Miaka iliyopita umoja wa watu botini umeshakinga maisha mengi!
- Bakia botini. Kila mwendo wa ghafla unaweza kuhatarisha watu botini: watu wanaweza kuanguka kutoka boti na boti inaweza kuzama! Kuna majambo mbalimbali ambayo wanawake na watoto walifungwa kebini chini ya ghorofa. Wakati huo huo mara nyingi kuwepo nje ni hatari, hasa kama hali ya hewa ni mbaya. Kwa hivyo ukiwepo kebini angalia inatokea nini nje na unaweza kwenda nje kwa haraka.

## Kama kuna hatari au dharura baharini piga simu kupata msaada

Mkiwa na dharura kubwa (kwa mfano bahari ina nguvu mno, boti yenu imeharibika au kupotea, mtu ametumbukia baharini) wapige watumishi wa mpaka papo hapo! Bila kutegemea uraia wako au hali ya kisheria yako, kuwako wato wanao dharura ni wajibu bila masharti kwa makepteni wote wa boti zote sawasawa kwa watumishi wa mpaka.

Wasiliane na watumishi wa ukombozi. Tumia namba zitakazofuata na jaribu kumtafuta mtu botini anayeongea lugha ya kinyeji au kiingereza.

Waeleze:

- kwamba mna dharura
- Mahali kwenu (GPS)
- idadi ya watu kwenye boti (wanaume, wanawake na watoto)
- hali ya afya za watu ambao ni wagonjwa
- ukubwa na hali ya boti yenu (maji yanaingia? Injini inafanya kazi bila matatizo?)

**Ugiriki:** +30 210 41 12 500

**Uturuki:**

+ 90 312 231 91 05

+ 90 312 425 - 33 37

+ 90 312 417 50 50 (Ukisikia sautu ya mashini ya lugha ya Uturuki bonyeza „O“!)

**International Idadi ya Dharura:** 112

Ukiwa na redio ya VHF botini, **tuma MayDay!** Maelezo ya kufanya hivyo utatafuta hapa: [www.wikihow.com/Call-Mayday-from-a-Marine-Vessel](http://www.wikihow.com/Call-Mayday-from-a-Marine-Vessel)).

**WatchTheMed Simu ya kin'gora**

**+ 334 86 51 71 61**



Namba hii siyo namba ya ukombozi lakini namba ya kin'gora kusaidia tendaji za ukombozi. Tuliunda namba hii pamoja na watendaji wa mashirika mbalimbali ambao wana umoja na wakimbizi na wahamiaji. Hatuna boti au helicopta kufanya tendaji/hatua za ukombozi. Kwa hivyo kwanza wapige watumishi wa mpaka. Kitu tunachoweza kufanya ni kuwafuata ili wajue kwamba tumeshapata habari na tunawaangalia wanachofanya! Msipookowa papo hapo au mkiwarudishwa tutajulisha uyombo uya habari na kupinga hivi.against this.

Unaposubiri kwa ukombozi au ukiona mwanga wa pwani au boti nyingine karibu, jaribu kupata uangalifu kwa kila namna (kwa kutumia roketi ya dharrura, kwa kutuma moshi ya rangi ya machungwa kutoka jerekeni, kwa kupunga na nguo zenye kun'gaa, kwa kutumia vioo, kwa kuwasha tochi usiku, kwa kupiga kelele, kwa kupiga mluzi, kwa kunn'gaa na simu au uyombo uya umeme vingine). Usiwake moto botini kupata uangalifu. Ukiwa na dharraru usijaribu kuokoa mizigo yako!

### **Mtu akitumbukia baharini au boti ikizama:**

- Mtu akitumbukia baharini simamisha boti papo hapo! Usipotee kuangalia huyu mpaka ameshaokowa! Tupa boya, kizibao au kiti kingine kinachoweza kuelea kwa mtu huu papo hapo. Fanya unachweza kufanya bila kuhatarisha maisha yako.
- Mmoja baharini anaye kizibao cha ukombozi ajiweke katika msimamo wa kijusi au aelee mgongoni asipokuwa na kizibao. Baadhi ya watu baharini wanao kizibao waungane na watu wengine kupata usawa na kupasha joto au waelee mgongoni watu wote kufungwa wasipowa na vizibao.
- Mtu akirudi botini, chukua nguo zake mkaushe na mfunike na blanketi! Kama hakuna kupumua, mfunge mdomo wake, puliza katika pua yake na tumia ukandaji wa moyo!
- Boti ikipinduka kabisa jaribu kushikilia botini au sehemu za kuelea!

### **Wakati wa ukombozi: kuwa na ululivu!**

Mkiokowa na boti nyingine, ukae na usisogee ghafla botini kwa ajili ya hatari ya kupinduka. Ukitaka kuomba kwa hifadhi ya kisiasa sema hii kwa udhahiri. Mwambie kepteni kwamba una uwezo wa kupata hifadhi ya kisiasa ukiiomba na mwombe kukupeleka bandarini nchini salama ambapo hutatishiwa.

#### **WatchTheMed Simu ya kin'gora**

[www.alarmphone.org](http://www.alarmphone.org)

[www.facebook.com/watchthemed.alarmphone](https://www.facebook.com/watchthemed.alarmphone)

[twitter.com/alarm\\_phone](https://twitter.com/alarm_phone)

mawasiliano: [wtm-alarm-phone01@antira.info](mailto:wtm-alarm-phone01@antira.info)

## **Fasili ya ufukuzaji wa pamoja (Push-Back)**

Kurudishwa kwa nguvu ni ufukuzaji wa pamoja ambao ni marufuku katika sheria ya kimataifa. Ufukuzaji wa pamoja ni kila hatua inayowalazimisha wageni, kama kikundi, kuondoka nchini kabla ya uchunguzi wenye sababu maalum wa kesi fulani ya kila mtu wa kikundi kile. Ibara 19 ya EU Charter ya haki maalum inakataza ufukuzaji wa pamoja. Haki hii imeharibikwa wakati ufukuzaji unatokea. Kila mtu anafaidi ulinzi dhidi ya ufukuzaji, pia watu wanao hali isiyo hakika/ya haramu. Marufuku ya ufukuzaji wa pamoja ni halali kwa maeneo yote kabisa ya nchi na maeneo ya bahari yake pia.

## **Ufukuzaji wa pamoja**

Kulikuwa na baadhi ya ripoti kuhusu ufukuzaji wa pamoja Uturuki (angalia sanduku kuona fasili ya ufukuzaji wa pamoja). Ufukuzaji sio haramu tu, lakini ni ya hatari kwa maisha ya watu. Kwa hivyo jaribu kutulia na kulinda maisha yako na ya watu wengine botini. Kama kuna hatari ya maisha au dharura usisite kupiga simu kupata msaada, bila kutegemea kwamba ina maana kukamatwa na watumishi wa Uturuki. Pia, jaribu kukumbuka na kusanya kila unagana unoyasaidia kutambua boti na watumishi wa mpaka kama namba za boti, rangi za boti au kila kitu kinachoeleza sura za watumishi.

## **Kuharibu boti**

Wakati uliopita walipendekezwa kuharibu boti yao wakati wanakamatwa na watumishi wa pwani wa Ugiriki ili wasifukuzwe Uturuki kwa sababu sheria inasema watumishi wanawajibikwa kuokoa maisha yenu ukiwa na hatari. Bali hatua hii ni hatua hatari sana na ilisababisha vifo vya watu wengi. Haku-na dhamana kwamba hamtafukzwa mkiharibu boti yenu. Na sheria ina sema mtu anayeharibu boti anaweza kushtikiwa kwa kuhatarisha maisha ya watu.





# UKIFIKA MAENEO YA UGIRIKI

Ukihitaji brosha inayoweza kukusaidia wakati unafika Ugiriki angalia maelezo Website ya „Welcome to Europe“ (Karibuni Ulaya) hapo:

<http://wzeu.info/greece.en/articles/greece-guide.en.html> (Brosha imeandikwa lugha ya kifarsi, kiarabu na kifaransa).

## Kuepuka fukuzaji wa Ugiriki

Kuna baadhi ya ripoti za fukuzaji zilizotokea wakati watu wameshafika Ugiriki. Kuepuka hivi kama bado kuna giza subiri mpaka mchana kabla mnaenda kwa watumishi. Lakini kama kuna watu botini wanaojeruhiwa au wasiohisi vizuri, pigia namba ya gari la wagonjwa (namba: 166). Kumbuka kwamba kuna maeneno makubwa ya visiwa uya Ugiriki ambapo hakuna watu wengi, kwa hivyo unaweza kupotea njia rahisi na kusafiri bila kumkuta mtu kwa masaa mengi. Jaribu kwenda mahali ambapo kuna watu. Ni muhimu sana kwamba watu wangi wanakuona, ili hatari ya ufukuzaji ipunguze. Wasiliane na watumishi kwamba mpo kisiwani baada ya kufika eneo changamfu. Mpaka mnakamatwa na mkaandikishwa kukupeleka kwa basi, teksi au gari kukatazwa kwa raia wa Ugiriki kwa sheria.

## Kuomba kwa hifadhi ya kisiasa

Ulivuka mpaka haramu. Tendo hilo ni marufuku kufuatana na sheria. Lakini unaruhusiwa kuomba kwa hifadhi ya kisiasa wakati wote na kuwa na uwezo

### Haki ya hifadhi

Kaidia ya Geneva 1951 inasema kuhusu hali ya wakimbizi kwamba istilahi ya „mkimbizi“ ni kila mtu ambaye ni nje ya nchi yake kwa ajili ya hofu kunyanyaswa kwa sababu ya rangi, dini, uraia, uanachama wa kikundi cha kijamii fulani au maoni ya kisiasa yake na hawezi au kwa ajili ya hofu kubwa hataki kudai ulinzi wa nchi yake au mtu ambaye hana uraia na ni nje ya nchi ya maskani ya mwisho na kwa ajili ya matokeo yale hawezi au kwa ajili ya hofu kubwa hataki kurudi. (Aya 1A)

kupata kesi ya hifadhi ya kisiasa yenye kufaa. Kuomba kwa hifadhi ya kisiasa Ugiriki lazima ufikishe mwenyewe ombi la hifadhi ya kisiasa kabla ya ofisi yenye kuhusika. Ofisi hii ni ofisi ya hifadhi ya kisiasa (kisiwani cha Lesvos, Rhodes, South na North Evos Region, Athen, kambi ya mahabusu ya Amygdaleza, Thessaloniki na Patras). Kwa maelezo kuhusu kesi za hifadhi ya kisiasa, unweza kupiga (kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa wakati wa kazi tu): UNHCR: 0030 – 210 – 67 26 462/3; Baraza ya Ugiriki kwa wakimbizi: 0030 210 – 38 00 990; Programu ya wakimbizi wa kanisa: 0030 210 72 95 926. Ukiwekwa ndani au kambini ya kupokea ya kwanza watumishi wataandikisha hiari yako kupata ulinzi wa kimataifa na watakuongoza kwa watumishi wa kuomba hifadhi ya kisiasa. Kupata orodha ya mashirika Ulaya na maelekezo kuhusu kesi ya hifadhi wa kisiasa, anagalia tovuti hii: **[www.wzeu.info](http://www.wzeu.info)**

## Kuingia haramu, kuandikisha na kuwekwa ndani

Kwa kuwa uliingia Ugiriki bila ruhusa inawezekana polisi itakuweka ndani. Visiwani uya Ugiriki kuna kambi ya kupokea ya kwanza moja (Moria/Mytilene) na kambi ya uchunguzi mbili (Samos na Chios). Kambini hizi utandikishwa na utakupa alama ya kidole. Kambini ya mahabusu wakati wa kifungo ni tofauti sana kutegemea ulifika wapi, kambi ina watu gani na kadhalika. Kambini ya kupokea ya kwanza kwa kawaida usikae zaidi ya siku 25. Lakini inawezekana kwamba utapelekwa kambini nyingine. Kambini ya mahabusu unaweza kuwekwa ndani hadi miezi 18 (mara chache hata zaidi) ukiwa na miaka zaidi ya 18. Lakini kwa kawaida wakimbizi wanawekwa ndani kidogo zaidi ya miezi 18 (muda wa kifungo inategemea idadi ya watu wanaofunga kambi wakati huo). Watoto na vijana (kati ya miaka 1 – 17) wasifunge kufuatana na sheria. Hata hivyo wanakaa kambi ya mahabusu mpaka watumishi wanawatafuta mahali pa kukaa kambi wazi kwa watoto, kwa kawaida kwa siku chache mpaka miezi mitatu. Ukiachiliwa, watu wazima watapokea „hati nyeupe“ kutoka polisi. Hati ile inasema uondoke Ugiriki na urudi nchi yako si zaidi ya siku chache mpaka siku 30. Hati ile siyo hati ya kusafiri au ruhusu ya kukaa. Inakulinda dhidi ya kukamatwa kwa wakati fulani (kama hati inayosema) usipoenda miji ya Patras au Igoumenitsa. Ikikwishwa unahatarisha kukamatwa tena. Ukiwa na miaka kidogo zaidi ya 18 hati ile hataisha mpaka utakuwana na miaka 18. Ukitoka Syria utachiliwa baada ya muda mfupi baada ya kuandikishwa na kutambuliwa kama raia wa Syria. Raia wa Syria wanapewa „hati ya kufuta ya kufukuzwa“, ambayo ni halali kwa miezi sita (kutoka tarehe ya utoaji) na inawezekana kuongeza muda wa hati hiyo.

# UKIFUKUZWA ENEO YA UTURUKI

Ukifukuzwa kurudi Uturuki au kuwekwa ndani na watumishi wa Uturuki inawezekana kwamba utawekwa ndani kambini ya mahabusu kwa baadhi ya siku (muda ya kuwekwa ndani inategemea sana lakini kwa kawaida ni muda mfupi tu). Muda wa kuwekwa ndani inategemea kwamba umesha-wekwa ndani na watumishi wa Uturuki na pia kwamba uliandikisha kwa hifadhi ya kisiasa au siyo. Inategemea mahali pa kuwekwa ndani pia. Laki-ni inawezekana kwamba watumishi wa Uturuki hawawakamata wakimbizi bali wanawaachilia. Ukiwekwa ndani unaweza kutafuta msaada wa kisheria hapa: Multeci Der in Izmir, Uturuki ((+90 232 483 54 21) au Helsinki People Assembly Istanbul ((+90 212 292 68 42 or +90 212 292 68 43).

## Ripoti kuhusu vifo vyote na kiukaji za haki zenu

Watu wakikufa au wanapotea botini au ukipoteya jamaa na unataka kuwa-tafuta, lazima uripoti hiyo watumishi waliokuweka ndani, na pia waambie hiyo Red Cross Athen (+30 210 8259002) na UNHCR (+30 2106726462/3).

Kama mlikuwa na dharura na boti ilikosa kutimiza wajibu wake kukuokoa ambapo watu wa boti wanaona hali yenu au mkifukuzwa kurudi na watumi-shi wa Ugiriki au polisi ya mpaka ya kimataifa tuma taarifa: [contact@w2eu.info](mailto:contact@w2eu.info) au [info@watchmed.net](mailto:info@watchmed.net)

Tunatumaini kusanya shahidi zenu na kuwahukumu watu wenye wajibu ili hali hizi hazitatrudia. Jaribu kupa naganaga zote unazokumbuka, na tutume picha au filamu zote kuhusu kivuko chenu. Utambulisho wako hautafunua na ushahidi wako ni bila kutambulika.



**welcomezeurope** ([www.w2eu.info](http://www.w2eu.info))

**Watch the med** ([www.watchthemed.net](http://www.watchthemed.net))

